Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 7, Issue 4

22nd Rabee ul-Awwal 1432

25th February, 2011

YANAYOHUSIANA NA MIKASA YA EGYPT

Mtayarishi: Sheikh Mash-hoor Hasan Aal-Salmaan (حفظه الله)

Yaliyomo

MIKASA YA EGYPT 1 - 4

JEE IBLEES ALIKUWA NI MALAIKA 4

AMESEMA SHEIKH: [Darsa ya Sheikh ya Swaheeh Muslim siku ya al-Khamisi 3rd February, 2011 C.E]

"MKASA HUU NI ADHABU ILIYOWASIBU WOTE PASI NA KUEPUSHWA YOYOTE KUTOKANA NA UDHAIFU WA KILA MTU. MABADILIKO YENYE KUTOKEA KULINGANA NA SUNNAH YA ALLAAH, KWA MUJIBU WA HADITHI ZA MITUME AMBAZO MOLA WETU ALOTUHADITHIA, HAYALETWI KWA NJIA HII. AMA KUHUSU NJIA ZA MAPINDUZI NA MFANO WAKE, BASI HIZO NI KATIKA NJIA ZA WAKOMUNISTI, WAZALENDO WA UTAIFA, WANASIYASA NA WATU WENYE KUPENDA MAISHA YA KILIMWENGU. NA DINI (YA UISLAMU) HAINA MAFUNGAMANO YOYOTE NA MAMBO YALIYOTOKEA EGYPT. MAMBO YANAYOTOKEA HUKO NI WATU MADHAIFU WENYE KUHISI YAKWAMBA WAO WANAKANDAMIZWA WANAONYESHA MSIMAMO WAO."

Kumebaki masuali matatu na yote yanahusiana na matukio ya Egypt! Kijana mmoja akasema: "Natumai yakwamba unaweza kutubainishia sisi hukmu ya kisheriya inayohusiana na matukio yanayoendelea muda huu katika nchi yetu ya Egypt?"

Jawabu kutoka kwa Sheikh Mash-hoor (حفظه الله): "Wallaahi ni nchi ipendezayo na Wallaahi mimi nawapenda watu kwa ajili ya Allaah. Wao ni miongoni mwa Waarabu, na hili linawahusu Egypt pamoja na al-'Iraaq, na lau utaziondoa nchi mbili hizi (Egypt na al-'Iraaq) kutoka kwenye ramani ya Nchi za kiarabu basi ni nadra kwa nchi zilizobaki kujimudu, kulingana na lugha ya uhariri wa kinadharia, yakiwemo ndani ya mipaka. Wakitakacho kwa Egypt ni sawa na walichokitaka kwa al-'Iraaq kwani walitaka maovu makubwa kwa al-'Iraaq na jambo la kushangaza ni kwamba wale walokusudia uovu kama huo kwa Egypt ni walewale walioiangamiza al-'Iraaq, hili ni jambo la kushangaza mno. Njama dhidi ya Egypt ni kongwe na Allaah Ana Sunnah katika Ulimwengu na hukmu zake za kisheriya. Mapinduzi ya watu wa Egypt yanakukumbusha wakati Allaah aliposema: **"Au ni nani ambaye atakupeni riziki kama Akizuiya riziki zake (Allaah)? Bali wao wanaendelea tu katika uasi na chuki."** [al-Mulk (67):21]. Kutokana na umasikini walio nao, na huku wakiwa ni wakaidi, na jeuri na walikuwa na chuki kubwa za kuendelea. Wale walioandamana walikuwa ni wenye jeuri nyingi na hali zao ni za kushangaza kwani kiongozi wao (Rais) alikuwa na miezi michache ya utawala na wanauliza iwapo hilo lilikuwa ni Halaal au Haraam na haliyakuwa walikuwa kimya!? Hili ni jambo la kushangaza sana. Hii inahusu maana ya maneno ya Allaah aliposema: **"Bali wao wanaendelea tu katika uasi na chuki."** [al-Mulk (67):21].

Sunnah ya Allaah katika Ulimwengu ni kwamba Dhulma ni Ziza (wingi wa Giza) na mwenye kuwadhulumu viumbe, licha ya kwamba mapinduzi yao si jambo ambalo Hukmu ya kisheriya inaruhusu, utatukuta sisi hatutekelezi jambo lililokatazwa kwenye Hukmu ya ki-Sheriya kama jambo ambalo lisokuwepo na lisotambulika. Michafuko inayotokea na mapinduzi haya hairuhusiwi na kutokea kwa vita baina ya makundi tafauti, ambayo matokeo yake yamezalisha hivi karibuni, ni mambo ya hatari kubwa. Misimamo ya watu wa kawaida ambayo hutegemea matangazo ya vyombo vya habari ina maana yakwamba wao wanaoleya kwenye mzingo walioangatishiwa, hili ni iwapo wao watafahamu au laa. Hairuhusiwi kwa mtu wa kawaida kufuata hukmu kutokana na msingi wa vyombo vya habari! Kwani vyombo vya habari huwa na njama, hupanga na huwasilisha hali kwa njia maalum ili wasikilizaji nao wahamasike kwa mujibu wa walichokihamasisha. Al-Hassan al-Basree amesema, kama ilivyo kwenye *al-Hilyah* cha Abu Nu'aim: "Fitna inayokuja hutambuliwa na mwanachuoni peke yake, na pindi ikishapita, hapo ndipo hutambuliwa na mwanachuoni pamoja na mjinga." Yanayotokea hivi sasa kwenye nchi ipendezayo ya Egypt hayana jengine isipokuwa ni kuangamiza mazuri yaliyobaki yaliyomo ndani ya nchi hiyo (ya Egypt). Kwani mashirika mengi ya Utangazaji, vyama vya ki-Siyasa na wenye mamlaka ya kuhukumu ni wenye kusababisha mifarakano wapate kuwagawanya watu wawe ni mapote tafauti, hapana shaka ni katika uenezaji mbaya kabisa wa fitna. Tunamuomba Allaah awahifadhi watu wa Egypt, Ailinde nchi yao na kwamba mja mwema achukuwe utawala wa nchi yao. Sisi hatupendezwi na hali

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

YANAYOHUSIANA NA MIKASA YA EGYPT

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

waliyo nayo sasa hivi, na hatukupendezwa na waliyoyafanya (ya maandamano na upinzani). Ni wajibu juu yao kujua yakwamba (mkasa) huu umetokea kwa ajili ya madhambi yao na kasoro walizo nazo. Vilevile ni jambo la kushangaza kuona yakwamba watu wa Egypt wanampenda Allaah sana na wanaipenda Dini Yake, lakini ni watu wenye hamasa sana na hawafahamu anayoyataka Allaah. Mkasa huu ni adhabu kwa wote pasi na kumuepuka yoyote kutokana na kasoro walizo nazo. Mabadiliko yenye kulingana na Sunnah ya Allaah, kwa mujibu wa hadithi za Mitume ambazo Mola wetu ametutajia, hayapatikani kwa njia hii. **"Hakika Allaah habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo katika nafsi zao."** [ar-Raad (13): 11].

Amma kuhusu njia za ku'asi na mfano wake, basi hizi ni njia za wa-Komunisti, Wazalendo wa U-Taifa, wana-Siyasa na watu wenye kupenda maisha ya kilimwengu. Amma kuhusu njia zinazolingana na Hukmu za ki-Sheriya, ambazo humlinda mtu chini ya kivuli chake, hii ni njia inayomuhusu kila mmoja wetu katika kubadilisha yale yaliyomo ndani ya nafsi zetu na juu ya kila mmoja wetu katika kutubia kwa Allaah kutokana na makosa yetu na kumnusuru Allaah kwa kumthibitisha mtu na vitendo vya wajibu kwa ujumla. Hii ni maana ya maneno ya Allaah: **"Enyi Mlioamini! Mkiinusuru Dini ya Allaah, naye Atakunusuruni na ataithubutisha miguu yenu."** [Muhammad (47): 7].

Ama kuhusu hali zetu kubakia kama zilivyo na Mola wetu, na madhambi yetu yakidhihiri, na vitendo vyetu viovu vikienea bila ya hata kujificha, na kisha tukitaka Allaah alete mabadiliko kwa kupitia kwetu sisi – basi haya ni malipo ya kusambaratika juu ya nafsi zetu na huku si katika kuisaidia Dini yetu. Dini haina mafungamano yoyote na mambo yanayotokea Egypt, kwani yanayotokea Egypt ni watu madhaifu wanaojiona yakwamba wanaonewa na kwahiyo wakaamua kuwa na msimamo, haliyakuwa wanavyuoni hawakuwa na mafungamano yoyote na yenye kutokea hapo. Ni waajib juu ya du'aat, 'Ulamaa na wanafunzi wa ki-Ilimu kuwatanabahisha watu kuhusu hatari zilizowakabili.

Sasa, mpaka Mamluki na wevi wamehusika waliotajwa na vyombo vya utangazaji kama "al-Baltajiyyah" au baadhi ya mapote miongoni mwa jeshi na watu walokodishwa. Wanasababisha mapote mawili kuwa na migogoro baina yao: *"Shaytaan amekata tamaa kutokamana na kuabudiwa ndani ya Bara-Arabu, hatahivyo husababisha tahreesh (mashambulizi ya mara kwa mara)."* Zogo hili na mashambulizi huanza na kurusha mawe, na leo imenifikia mimi yakwamba kumetumika mpaka risasi. Twamuomba Allaah ailinde Egypt na watu wake kutokamana na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Egypt ni nchi maskini na jamii nyingi hungojea kupokea mishahara ya siku hadi siku nyengine na lau kama hali hii itaendelea utakuta makumi, au hata mamia ya jamii watakaoshindwa kupata chochote cha kula. Umasikini ni Ukafiri, **"Umasikini ulikurubia kuwa Ukafiri"** kama ilivyonasibishwa kwa 'Ali **(** رضي الله عنه**)**. Sasa vitendo vilivyo kinyume (cha Hukmu za ki-Sheriya) viko wazi, Waume kwa wake walio *Mutabarrijaat* wamekaa na wameiwacha misikiti, wakiswali nje, bila ya kuzisitiri sehemu zao za siri, wakilala nje n.k (*na kadhaalika*). Kwahiyo kuna mchanganyiko wa halaiki ambao Hukmu za ki-Sheriya hazikuweza kuzingatiwa mahali hapo. Kwahiyo yoyote atakae Hukmu za Ki-Sheriya (Hukm Shar') kutoka kwetu na ajue yakwamba msimamo wa watu ni matokeo yakuhamasishwa na vyombo vya Utangazaji, kwahivyo, hatuna zaidi ya kuwausiya watu wote wamche Allaah na kila mmoja wao anawajibika kujua yaliyo wajibu juu yao na kwamba watu wasiuwawe au wasivurumizwe kwenye janga la vita na Vyombo vya Utangazaji. Watu na wajue iwapo wanamuabudu Allaah kwa vitendo kama hivyo (kwa kutegemea yale wanayoyapata kutoka kwenye Vyombo vya utangazaji) kisha kuna ushahidi gani ulioandikwa wa hilo? Hilo limetegemezwa juu ya nini? Na ni nani aliyewapa fatwa ya kuwaruhusu kufanya hivyo? Haifai kwa mtu wa kawaida kujitolea fatwaa yeye mwenyewe na hairuhusiwi kwa mtu wa kawaida kujidhania kuwa ni Mujaahid katika mahali pasipo na Imaam, na bila ya kumtegemea Imaam wala dalili ya maandishi. Na katika yaliyotokeza kutoka kwenye fataawa yamekuja kutoka kwa ambao wao wenyewe ni wasomi.

SUALI LA PILI:

"Jee inaruhusiwa kufanya Qunut na kuwaombea Du'aa' watu wa Egypt katika wakati kama huu?"

JAWABU: Naam, amma kuhusu matukio ya Egypt si jambo linalowahusu pote maalum au idadi chache ya watu, bali ni lenye kuwahusu watu wote kwa ujumla. Iwapo sisi tutawaombea basi na iwe ni kwenye swala tano za kila siku. Imaam na walio nyuma yake watainua mikono yao na Imaam ataomba Du'aa' na walio nyuma yake wataitikia 'Aameen'. Maombi yenyewe yawe ni kumuomba Allaah aondoe maafa kutoka kwa watu wa Egypt, azihifadhi damu zao, mali zao, heshima zao na Waislamu wote walio juu ya ardhi hii na chini ya mbingu zote. Maafa haya yaliyowasibu watu wa Egypt, Wallaahi ni makubwa na mpangilio wa kawaida tuliouzoea tangu mwanzoni mwa fahamu zetu mpaka sasa ni kwamba njama zilizowekwa kuushambulia Ummah huanzia dhidi ya Egypt na kisha njama hizi husongea kwa watu wengine baada ya Egypt. Namuomba Allaah ayakate mizizi ya fitna hii na namuomba Allaah asija'alie fitna hii kusambaa na kuingia kwenye miji mengine ya Waislamu. Vikundi vilivyo nyuma ya mambo haya vinaweza kuambukiza wakati wowote wapendapo na kwenye nchi yoyote wapendayo na wana uwezo wa kutengeneza njia kwa hayo. Zaidi ya hayo, kila mtu mwenye akili anajua yakwamba kwa wale (wenye

YANAYOHUSIANA NA MIKASA YA EGYPT

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

kuandamana) inaruhusiwa kwangu kuwasifu wao kama watu 'maskini' (Masaakeen) na naweza kuongeza juu ya kuwasifu kwangu kuwa wao ni maskini kwa kusema pia yakwamba wao ni "wakweli" (Saadiqeen). Mimi nawazingatia wengi wao kuwa ni wakweli ingawaje wao ni masaakeen. Wao hawayajui haya wala hawaelewi kuyahusu haya tuyasemayo (kwa sasa), lakini baada ya miaka michache watakuja kujua yakwamba walikuwa kwenye udanganyifu na walikuwa wamedanganywa. Sasa sisi twasubiri kitu gani? Kwani wao wanatarajia nini? Baada ya kusononeka na machungu kujidhihirisha, ni yapi yalopatikana? Maisha, damu na sehemu za viungo, yote hayo yalikosekana na watu walodhurika kwa kuwa vilema, umasikini na kupoteza mali zao. Umasikini ulikuwa tayari ushajitokeza na vitendo vyao ni vyenye kuizidisha Egypt kwenye ufukara, na mgawanyiko upo na yaliyotokea yamewazidishia mgawanyiko.

Wakati umefika kwetu sisi kuyasema maneno yetu na kuwajulisha watu yakwamba tafauti ya kwanza kwenye Ummah huu imetokamana na kukhitilafiana katika ufahamu na haliyakuwa umoja tunaoulingania, kabla ya kuunganishwa kwa makundi, hapana budi yafungamanishwe katika ufahamu. Ikhtilafu ya kwanza kwenye kanuni za Imaan ilijitokeza baada ya zama za 'Umar Ibn al-Khattaab (رضي الله عنه) kama alivyotueleza Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم). Amepokea Imaam al-Bukhaari kwatika swaheeh yake kutoka kwa Abu Waa'il Shaqeeq Ibn Salamah aliyesema: "Tulikusanyika kwenye kikao pamoja na 'Umar Ibn al-Khattaab (رضي الله عنه) mara akasema 'Umar: 'Ni nani miongoni mwenu aliyehifadhi hadeeth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) inayohusiana na fitna?' Akajibu Hudhayfah: 'Mimi nimehifadhi ewe kiongozi wa waumini.' Akasema 'Umar: 'Hebu tusimulie hadeeth yenyewe, kwani kwa hakika wewe ni mjasiri (shujaa).' Hudhayfa akasema: 'Fitna ya mtu katika jamii yake, mali yake, nafsi yake, mtoto wake na jirani yake. Yote hayo kafara yake ni (husamehewa kwa) swala, swadaka, kuamrisha mema na kukataza maovu.' 'Umar (رضي الله عنه) akamjibu: 'Mimi sikukusudia kukuuliza kuhusu hayo (sampuli hiyo ya fitna).' [*Kwahivyo, fitna za sampuli hiyo hazitowacha kuwepo miongoni mwa watu katika maisha yao yote*]. 'Bali mimi nakuuliza kuhusu fitna ambayo itakayosababisha mapinde kama mawimbi baharini.' [*Kama mikasa yanayotokea huko Egypt hivi sasa na pia ni mfano tu wa yanayotokea al-'Iraaq*]. Hudhayfah akasema: 'Sasa una lipi la kufanya kuhusiana na haya ewe kiongozi wa waumini? Kwani baina yako wewe (na hiyo mikasa) kuna mlango.' 'Umar akamuuliza Hudhayfah: 'Kwani huwo mlango uko wazi au umevunjika?' Akajibu Hudhaifah: 'Kwa hakika mlango umeshavunjika.' Akasema 'Umar: 'Wallaahi, (mlango) huwo hautoweza kufungika milele.'" Na 'Umar alikuwa akijua yakwamba yeye ndiye mlango huwo.

Ni kama kwamba hiyo fitna imefungiwa ndani ya chumba na 'Umar Ibn al-Khattaab (رضي الله عنه) ndiye mlango, kwahivyo ikiwa yeye alikufa kifo cha kawaida bila ya kuuliwa, basi mlango ulio wazi unaashiriya mikasa iliyouzunguka Ummah ambayo pana uwezekano wa kuufunga. Lakini mlango ulovunjwa haukufunguliwa (kama unavyostahiki). 'Umar aliuliwa na wala hakufa (kifo cha kawaida). Matokeo yake, mikasa itabaki kuuviringa Ummah mpaka siku ya Malipo na hauwezi kufungwa. Huu ndiwo mkasa tunaoushuhudia ambao 'Umar na Hudhayfah (رضي الله عنهم) waloukusudia. Salamah Ibn Shaqeeq alisema: "Tulikuwa tukiogopa kumuuliza 'Umar iwapo alikuwa akijua yakwamba yeye ndiye mlango ulokusudiwa, kwahivyo tukamuuliza Masrooq Ibn al-Ajda' atuulizie badala yetu nae Masrooq akatwambia: 'Na'am, Wallaahi, mkusudiwa hapo alikuwa ni 'Umar. Alijuwa yakwamba yeye ndiye aliyekuwa mlango kama ajuavyo yakwamba usiku huuleta mchana wa siku ifuatayo.'"

Mikasa hii yenye kusababisha mapinde kama mawimbi baharini yalianza baada ya kuuliwa 'Umar Ibn al-Khattaab (رضي الله عنه) kutokana na mikasa ya ma-Khawaarij na Rawaafidh. Kwa yote hayo, nakusudia yakwamba migawanyiko miongoni mwa Ummah yalizagaa kutokana na ufahamu uliotafautiana, kwahiyo ni jambo la lazima kwa Ummah mzima, kabla ya kulingania kwenye umoja, wajaribu kuvuna ufahamu ulio swaheeh na wawe na malengo juu ya maamrisho na chimbuko la ufahamu wao. Amma kuhusu kuinuka kwao, wakitarajia na kutafuta haki zao kwa njia za jeuri na kukirihishwa na mifumo, bila ya kuungana katika ufahamu wao kulingana na Hukmu za ki-Sheriya, na bila ya kujitegemeza kwa wanavyuoni, basi hayo si katika fungu la Allaah kwa hali yoyote iwayo. Ugomvi miongoni mwa watu unaohusiana na uongozi, mapato, mishahara, kupeana heshima na ubinafsi, ukiandamana na watu wanaohisi hali za maonevu, ufukara wa hali ya mwisho na njaa, yamemaanisha yakwamba kuna sababu chungu nzima zenye kuchangia haya matukio tunayoyaona. Tunayoyaona ni mchaganyiko ulokusanya Ziza (wingi wa Giza) na vitendo vilivyo kinyume (cha Hukmu za ki-Sheriya) na iwapo sisi twataka kuwaondolea maafa haya Ummah basi itatubidi kuelekeza ulinganizi wetu kwa mapote yote husika pasi na kuelekeza kwa mmoja bila ya mwengine. Mambo yanayotokea hayatoleta mazao yoyote kama kutapatikana jawabu au kusipatikane na kama Rais (kiongozi) atabadilishwa au asibadilishwe, kwa sababu hayo hayakutegemezwa katika kuinusuru dini na kuitangaza haki kwa sababu mtindo wa mabadiliko haukwenda sambamba na Sunnah ya Allaah katika Hukmu zake za ki-Sheriya. Mabadiliko kulingana na watu wenye kuyapenda maisha ya kilimwengu na kanuni zao za mifumo ya mapinduzi, kuandamana na ku'asi huleta mabadiliko kwa

... MIKASA YA EGYPT

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

haraka lakini hayawi ni yenye kutegemezwa juu ya kuitangaza dini na haki au kudumu katika kuitangaza dini na haki. Baadhi ya madai ya maisha ya kilimwengu hwenda yakajibiwa kwa kiasi cha watu wapate kuonja utekelezaji wa madai hayo. Kwahivyo, ni wajibu, ikiwa tunataka Mola wetu awe radhi na sisi, na iwapo sisi tunataka kuinusuru dini yetu, kuzibadilisha nafsi zetu kwanza: **“Hakika Allaah habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo katika nafsi zao.”** [ar-Ra’d (13): 11]

Aya hiyo inafahamisha ukanushaji (laa) na neno “Qawm” hapa halina mipaka kwahivyo mfumo huu unakuwa kwenye misemo ya ujumla (Al-faadh ul-‘Umoom) na kwahiyo, inawahusu watu wa Egypt na watu wengineo pia. Kusudio la “mabadiliko” hapa ni mabadiliko kulingana na hukmu za ki-sheriya na Allaah ametaja mabadiliko sampuli mbili: mtendaji wa mabadiliko ya kwanza, ambaye ni Allaah na pili: mtendaji katika mabadiliko ya pili ni mtu ambaye anayepaswa kubadilisha kila kitu kilichomo ndani yake. Allaah ametegemeza Kitendo chake kulingana na Sunnah ya Hukmu Zake za ki-sheriya ya kuwabadilisha watu pindi watakapojibadilisha nafsi zao. Mabadiliko yatokeayo hivi leo ni kulingana na Sunnah ya Allaah peke yake na Ulimwengu Wake na wala si kulingana na Sunnah ya Allaah na Hukmu zake za ki-Sheriya. Ni wajibu wa wanavyuoni kufanya bidii wajitahidi katika kufanikisha mabadiliko yanayolingana na Sunnah ya Allaah na Hukmu zake za ki-sheriya. Wanapaswa kuwafundisha watu na kuukusanya ufahamu wao juu ya Hukmu Takatifu za ki-sheriya kulingana na maandiko yaliyo kwenye Kitaab, Sunnah na ufahamu wa Salaf wa Ummah huu. Iwapo kutakuwa na umoja katika ufahamu, basi Umoja wa miili yao utafuata kwa wepesi na pia patapatikana majibu ya haraka kwenye mafunzo ya Hakimu Mkuu Allaah (عزّ وجل). Haya ni maneno yangu kuhusiana na matukio yanayoendelea huko Egypt.

JEE, IBLEES ALIKUWA NI MALAIKA?

Kuhusiana na maneno ya Allaah (شبحانه وتعالى) (kama yalivyofasiriwa):
"Na (wakumbushe watu khabari hii): Tulipowaambia Malaika: "Msujudieni Adam." Wakamsujudia wote isipokuwa Iblees; akakataa na akajivuna; na alikuwa katika makafiri." [Soorah al-Baqarah 2:34]
Kuna baadhi ya watu wanaosema, kulingana na aya hii, yakwamba Iblees alikuwa ni Malaika. At-Tabaree ni miongoni mwa wenye rai kama hii, akasema: "Hakuna pingamizi yoyote katika wazo hili yakwamba Allaah (شبحانه وتعالى) angeweza kuumba jamii ya Malaika Wake kutokamana na chochote katika vile alivyoviumba, kwani pana uwezekano yakwamba aliiumba jamii ya Malaika, akiwemo Iblees miongoni mwao, kutokamana na moto, na tena Iblees alikuwa na maumbile yasiyo na kifani, tafauti na Malaika wengine, kwa kuumbwa kwake na moto wa *Samoom*." Hatahivyo, rai hii imepingwa na jamhuri ya Wanavyuoni, wakiwemo miongoni mwao Ibn Katheer aliyesema: "Amma yeye (huyu Iblees) aliumbwa kutokamana na moto usiotoa moshi na Malaika nao wakaumbwa kutokamana na muangaza kama ilivyopokewa kwenye hadeeth swaheeh katika Swaheeh Muslim, kutoka kwa bibi 'Aaisha (رضي الله عنها) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Malaika wameumbwa kutokamana na muangaza na Iblees ameumbwa kutokamana na Moto usiotoa moshi... Alikuwa akitekeleza huduma za Malaika mpaka akawa amefanana nao hata katika kumuabudu [Allaah (شبحانه وتعالى)] na kujitolea kwake kwa bidii. Kwahivyo, alihusishwa kwenye ulinganizi wa Allaah (شبحانه وتعالى) kwao (mwito wa kumsujudia Adam) nae akakataa kwa majivuno."*
Na akaendelea Ibn Katheer; Allaah (شبحانه وتعالى) ametaja hapa yakuwa Iblees ni miongoni mwa Majini - yaani, ameumbwa kutokamana na moto, kama alivyosema Allaah (شبحانه وتعالى) (kama ilivyofasiriwa):
Akasema: "Mimi ni bora kuliko yeye. (Mimi) umeniumba kwa moto, naye umemuumba kwa udongo." [Soorah al-A'raaf 7:12]
Al-Hassan Al-Basree amesema: "Iblees hakujaaliwa kuwa miongoni mwa Malaika kabisa. Yeye alikuwemo miongoni mwa kundi la Majini, kama vile Adam (عليه السلام) alivyokuwemo miongoni mwa kundi la watu." (Hayo yamesimuliwa na Ibn Jareer kwa Isnaad iliyo swaheeh).
Ni muhimu vilevile hapa kueleza yakwamba Allaah (شبحانه وتعالى) Amesema (kama ilivyofasiriwa):
"Je! mnamfanya yeye [Iblees] na kizazi chake kuwa marafiki [zenu] badala yangu, hali wao ni maadui zenu...?" [Soorah al-Kahf 18:50]
Kama inavyojulikana na kila mtu, Majini wana uwezo wa kuzaa kama vile wanavyozaa binadamu, haliyakuwa Malaika hawazai. Na pia Malaika hawana khiyari; wao ni watiifu daima mbele ya amri za Allaah (شبحانه وتعالى), kinyume cha Majini ambao, kama binadamu, wamepewa vipimo fulani vya khiyari (uhuru wa kufanya watakavyo).
Akasema Allaah (شبحانه وتعالى) (kama ilivyofasiriwa) kuwahusu Malaika:
"Wanamuogopa Mola wao aliye juu yao, na wanatenda wanayoamrishwa" [Soorah an-Nahl 16:50]
Na Akasema tena Allaah (شبحانه وتعالى) (kama ilivyofasiriwa):
"Enyi mlioamini! Jiokoeni nafsi zenu na watu wenu, na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Wanausimamia Malaika wakali, wenye nguvu, hawamuasi Allaah kwa amri zake; na wanatenda wanayoamrishwa (yote)." [Soorah at-Tahreem 66:6].

Al-Hassan al-Basree amesema, kama ilivyo kwenye *al-Hilyah* cha Abu Nu’aim:

“Fitna inayokuja hutambuliwa na mwanachuoni peke yake, na pindi ikishapita, hapo ndipo hutambuliwa na mwanachuoni pamoja na mjinga.”